**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 07** **"Kwapikwa nini?"**

**Author:** **Njoki C. Muhoho**
**Medical Advisor** **Dr Ng'ethe Muhoho**
**Editor** **Maja Braun**

**Kisuaheli** **Eric Ponda**

<table>
<tr><th>Scene</th><th>Characters</th><th></th></tr>
<tr><td>1</td><td>1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. EDITH<br>4. MARIA</td><td rowspan="4">SAM – 17, m.<br>MARIA – 43, f.<br>EDITH – 40, f.<br>EDDI– 36, m.<br>DR SALLY – 34, f.<br>CHEMU – 15, f.<br>NARRATOR</td></tr>
<tr><td>2</td><td>1. MARIA<br>2. EDITH<br>3. MARIA<br>4. CHEMU<br>5. SAM</td></tr>
<tr><td>3</td><td>1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. EDITH<br>4. MARIA<br>5. NARRATOR</td></tr>
<tr><td>4</td><td>1. SAM</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| | 2. EDDI<br>3. EDITH<br>4. CHEMU<br>5. MARIA | |
| **5** | 6. SAM<br>7. CHEMU<br>8. EDDI<br>9. EDITH<br>10. MARIA | |
| **6** | 1 SAM<br>2 CHEMU | |

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** HUJAMBO NA KARIBU KWA SEHEMU YA SABA YA MFULULIZO WA VIPINDI VYA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO TUKIWA BADO TUNAZUNGUMZIA MASUALA YA USAFI NA JINSI NA KUJIKINGA NA UGONJWA WA KUHARA. KATIKA MAKALA ILIYOTANGULIA MARAFIKI WAWILI SAM NA CHEMU-BAADA YA KUKABILIWA NA HALI NGUMU YA UGONJWA WA KUHARA HATIMAYE WANAKUWA MABALOZI WA NIA NJEMA WA KUWAELIMISHA WENZAO UMUHIMU WA KUDUMISHA USAFI.MJOMBA EDDI, AFISA WA HUDUMA ZA AFYA YA JAMII PIA ALIKUWEPO KUWASAIDIA.NYUMBANI KWAO, WATOTO HAO WAMEFANIKIWA KUMSHAWISHI JIRANI YAO MARIA KUZIOSHA MBOGA NA MATUNDA KABLA YA KULA. NA SI HAYO TU, BADO KUNA MENGI YA KUJIFUNZA KATIKA FAMILIA HII.

KWA MENGI ZAIDI HEBU TUUNGANE NA SAM NA FAMILIA KUFAHAMU ZAIDI NJIA BORA ZA KINGA DHIDI YA UGONJWA HUU..

**SCENE 1: EDITH'S HOME**

**02.** ***SFX: HEAVY FOOTSTEPS. SEVERAL THUDS AS HEAVY PACKAGES LAND ON HARD GROUND.***

**03. SAM** Mama nadhani tumenunua chakula kingi sana ?.

**04. EDITH** Mwanangu kwani unamesahau kwamba nyumba hii watu wanakula chakula kingi kama mchwa. Chakula hiki kitamalizika katika kipindi cha wiki moja tu.

**05. CHEMU** Hata mamangu pia amekuwa na hamu ya chakula siku hizi na apenda tuwe tukila hapa siku zote.

**06. EDITH** Ni kweli Chemu lakini hakuna Mtu atakayetatizwa na njaa katika nyumba yangu, na urafiki wetu ni sawa na udugu. Mumelizungumzia.

**07. MARIA** suala la chakula, sasa nimesikia kiu sana Edith.

**08. EDITH** Sam, tafadhali mletee Shangazi Maria maji ya kunywa.

**09. SAM** Aaahhh… kuna tatizo…!

**10. MARIA** Ni nini tena…? hakuna maji. Yaani kuna chakula chote hiki na hakuna maji?

**11. SAM** Hapana…! Maji yaliyoko hayajachemshwa.

**12. MARIA** Ahhh, mimi sijawahi kuchemsha maji katika maisha yangu na afya yangu haina matatizo.

**13. SAM** Lakini shangazi, mambo yamebadilika….tunalifahamu suala vyema.

**14. MARIA** Hilo haliwezi kunizuia kuwa na kiu au kunywa maji. Niletee maji hayo haraka upesi…!

**15. CHEMU** Mama unakumbuka wale watoto waliokuwa wakijisaidia kando kando ya mto, kufua nguo na hata ngombe pia kukanyaga kinyesi na kisha kuingia kwenye maji hayo ya mto? Walisambaza vidudu vinavyosababisha kuhara…!.

**16. SAM** Na kisha bila ya kusahau, mvua zimekuwa zikinyesha na zikakisomba kinyesi chote tangu nianze kujisaidia katika shamba lako wakati nilipokuwa nikihara.Vyote nilivyoacha shambani mwako vimesombwa na maji hayo ya mvua hadi mtoni, na sasa ni maji hayo hayo unayotaka kuyanywa….yuuuk!

**17. MARIA** **Basi….. basi….**sasa komea hapo.. yachemshe maji hayo nitasubiri.Siutaki huo ugonjwa wa kuhara.

**18. EDITH** Kwa vile nyinyi watoto mumekuwa wataalam wa masuala haya, kwanini msiviandae vyakula hivyo vibichi kisha mimi na Maria tutavipika.

**19. CHEMU** Sawa kabisa.

**20. SAM** Hata mimi nitakusaidia…! Lakini kwanza tuvioshe.

**21. SAM** Tutaviosha na maji yaliyochemshwa..

**22.** ***SFX WATER FLUSHING (WASHING OF VEGETABLES*****)**

**23. CHEMU** Kisha tutavifuta maji yote.

**24. SAM** Hayo ni mambo rahisi.

**25. CHEMU** Sasa tuzikatekate nyama.

**26. MARIA** Nyie watoto, jihadharini na kisu hicho kikali…

**27. SFX CUTS OF KNIFE ON WOODEN BOARD**

**28. SAM** Sawa shangazi... tutakuwa waangalifu. Ahhh angalia nzi walivyojazana hapa. Nadhani walipata harufu kutokea nje. Wanaweza kuwa wana vile vidudu

**29. CHEMU** Tutaikata kata upesi kisha tuifunike.

**30. EDITH** Tufunike nyama? Kwa nini? Nilidhani tunaipika sasa hivi.

**31. SAM** **Kwasababu nzi wanahitaji dakika chache tu kuacha mayai na vidudu wanapotua kwenye nyama, tunapoila nyama hiyo tunakula uchafu huo pia!**

**32. EDITH** Nitahakikisha naipika hadi iive vizuri ili kuviua vidudu hivyo.

**33. SAM** **Sawa basi tuyafanye yote hayo.**

**BRIDGE MUSIC**

**<u>SCENE 2 EDITH DINING AREA</u>**

**34. *SFX: SOUNDS OF CUTLERY***

**35. MARIA** Mama Sam, chakula kilikuwa kitamu sana.!

**36. EDITH** **Sote tumeshirikiana kukipika chakula hiki, na sasa lazima pia tushirikiane kuviosha vyombo jikoni.**

**37. MARIA** ***(yawning)* Ahhh .. nimechoka sana…!.**Siku ya leo imekuwa na pilkapilka nyingi sana kwa kweli…!.

**38. EDITH** **Mimi pia nimechoka sana…!**

**39. MARIA** **Lakini bado hatujaosha vyombo…! Je muna fikira kama zangu**?

**40. EDITH** (***shouting across to Sam)*** Sam, Chemu! Viacheni hivyo vyombo kwenye beseni tutaviosha kesho.

**41. SAM** Hapana Mama... tutaviosha sasa hivi…! Tukiviacha hadi kesho, vitang'ong'wa na nzi na huenda tukakabiliwa na tishio la kuambukizwa ugonjwa wa kuhara.

**42. CHEMU** Shangazi... mimi na Sam tutaviosha!

**43. MARIA** Unajua nini? Kama watoto wote wangekuwa wana bidii kama hawa katika harakati za kuuepuka **ugonjwa wa kuhara, dunia ingekuwa mahala salama pa kuishi.**

**44. NARRATOR** MARIA ANASEMA KWELI. KAMA WATOTO WOTE WANGEJITOLEA KUDUMISHA USAFI WAO, HAPANA SHAKA TUNGEUPUNGUZA UWEZEKANO WA KUAMBUKIZWA UGONJWA HUU NA VIFO.

NI MAMBO MEPESI NA RAHISI AMBAYO YANAYORUDIWA KILA MARA KAMA KUWA NA MAZOEA YA KUNAWA AU KUOSHA CHAKULA KABLA YA KULA AU KUPIKA.

NI NJIA MUJARAB NA RAHISI KWA AFYA BORA.

BAADAYE SIKU HIYO SHEMEJIYE MAMA SAM EDDI AMBAYE PIA NI AFISA WA HUDUMA ZA AFYA YA JAMII KIJIINI HUMO ALIWATEMBELEA TENA: FAMILIA HIYO ILIKUWA BADO INA MASWALI MENGI

**BRIDGE MUSIC**

**SCENE 4: EDITH'S COMPOUND-OUTSIDE.**

**45. SFX** ***OUTSIDE SOUNDS: BIRDS, CRICKETS***

**46. SAM** **Mjomba Eddi, wakati madaktari waliponifanyia uchunguzi hospitalini walinifahamisha kuhusu vidudu na vimelea vilivyokuwa vikiishi tumboni mwangu.**

**47. EDDI** Ni kweli. Wakiwa katika maabara,… madaktari wanaweza kuviona vidudu hivyo.

**48. EDITH** Je ni kweli mtu yeyote anaweza kuambukizwa vidudu hivyo?

**49. EDDI** Ni kweli kabisa... Mtu yeyote anaweza kuambukizwa.

**50. MARIA** Hata kwa watu ambao wanadumisha hali ya juu ya usafi mfano kunawa kila mara, kuosha chakula na kuchemsha maji ya kunywa kama ilivyo kawaida siku hizi?

**51. EDDI** Hata kwa mtu anayedumisha kanuni hizo. Kumbuka pia unaweza kununua chakula mkahawani, kusalimiana na watu kwa mkono au kushika vitu. Hali hii inaihatarisha afya yako hata kama unadumisha usafi nyumbani.

**52. CHEMU** Basi itabidi sote tukafanyiwe uchunguzi.

**53. EDDI** Si wazo baya.

**54. MARIA** Lakini mimi si mgonjwa. Sijaambukizwa ugonjwa huo wa kuhara. Kwanini niende nikafanyiwe uchunguzi.?

**55. EDITH** Nadhani ni wazo zuri tu. Sote tunaishi katika mazingira ambamo vidudu na vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa kuhara vinapatikana. Mimi ningependa kupimwa.

**56. CHEMU** Hata mimi pia, mjomba Eddi. Je rafiki wangu shuleni pia wanaweza kwenda kupimwa?

**57. EDDI** Bila shaka tutapanga na mwalimu. Nataka kuja shuleni hivi karibuni.

**58. MARIA** Lakini kuna haja gani? Kama unasema unaweza kuviona vidudu hivi tumboni mwangu na havijanidhuru, kwa nini nivisumbue.

**59. EDDI** Usijidanganye…! Kama una vidudu basi ujue vinaendelea kukua pole pole tumboni mwako. Tumbo huwa mazingira bora kwa vidudu na Vimelea hivyo kunawiri. Baada ya muda mtu anaweza kuupata ugonjwa wa kuhara.

**60. MARIA** Sawa umeniogofya sana. Lazima nikapimwe pia.

**61. EDDI** Vizuri sana. Nimefurahi kusikia uamuzi huo.Nitaanyadaa mipango yote ili twende hospitalini kupimwa.

**BRIDGE MUSIC**

**<u>SCENE 5: HOSPITAL LABORATORY</u>**

**62. *SFX*** ***CLATTER OF TEST TUBES***

**63. NARRATOR** HAKUNA MTU ANAYEPENDA KWENDA HOSPITALINI.KWA KAWAIDA MTU ANAPOTEMBELEA HOSPITALI HUWA ANAUGUA AU KWENDA KUMUONA MGONJWA. LAKINI SASA NI TOFAUTI KABISA. SAM, FAMILIA YAKE NA RAFIKI ZAKE WAMEFIKA HOSPITALINI SIO KUTIBIWA BALI KUPIMWA IWAPO WAMEAMBUKIZWA UGONJWA WA KUHARA..KWANI …KINGA NI BORA KULIKO TIBA…!.

**64. EDDI** Sawa kila mmoja achukue kijichupa hiki kidogo. Katika chupa hiyo utaweka kiasi kidogo cha kinyesi chako kisha ukiregeshe..!.

**65. MARIA** ***(loud whisper)*** Wanataka ni…..ni…. weke katika kijichupa kile? Aibu gani jamani hiii?

**66. SAM** Shangazi Maria ….si jambo la aibu…! Kila mmoja hana budi kufanya hivyo…!

**67. CHEMU** Wewe unaogopa tu Mama. Unapaswa kulifurahia zoezi hili…!

**68. EDITH** Maria, swahiba yangu yangu hebu tushirikiane, ili tufanyiwe tu kwa heshima ya Fatu. Endapo mimi na wewe tungelijua mambo haya mapema, leo Fatu hangekuwa marehemu…!

**69. MARIA** Sawa basi tufanye kwa heshima yake.

**70. EDDI** Vyema basi. Hebu twendelee. Leteni sampuli zenu sasa.

**71. EDITH** Eddi sasa wakifanya uchunguzi… na wapate ….. kuna …,. Vile vidudu, watafanya nini baada ya hapo?

**72. EDDI** Endapo watavipata vidudu, basi ufahamu wewe ni mgonjwa, na hapo watakupa dawa ya kuviua.

**73. MARIA** Basi kama mwishowe mutatupa dawa kwanini kuyafanya mambo yote haya ya aibu …? Kwa nini hamtupi mfuko mzima tutumie kama familia bila ya kushiriki kwenye mambo haya ya aibu? Si mtupatia dawa hiyo mara moja twendeni nyumbani...! Mfuko mzima unatosha kutumiwa na familia nzima badala ya kupitishwe kwenye fedhehe hii

**74.**

**75. SAM** Shangazi si rahisi hivyo.

**76. CHEMU** Watu hawapaswi kugawana dawa!

**77. MARIA** Kwanini? Kama tunaweza kugawanya chakula… kwa nini sio Dawa?

**78. EDDI** Sawa... sasa ngojeni nimueleze. Hii ni la muhimu sana na msikilize kwa makini. Kila mtu hupewa dawa kulingana na uchunguzi wa ugonjwa au vidudu alivyoambukizwa tumboni.Dawa hiyo huwa ina masharti.

**79. CHEMU** Unamaana gani ukisema ina masharti?

**80. EDDI** Yaani kila mmoja hupewa dawa na anapasa kuyafuata maagizo aliyopewa na daktari. Kiwango na wakati uliopendekezwa hadi dawa hiyo itakapomalizika.

**81. MARIA** Na kama nasikia nafuu, kwanini niendelee kumeza dawa hizo? Kwanini nizimalize nitimize hilo….umesemaje vile….Shuruti…?

**82. CHEMU** Endapo hutamaliza dawa hizo, vidudu hivyo vitapata uhai na kuanza tena kuzaana tumboni, na hatimaye utaanza kuhara tena.

**83. EDDI** Sawa kabisa maelezo mazuri sana Chemu….! umeeleza vizuri…sasa… bado tuna kazi ya kufanya hapa, hebu tuendelee na shughuli hiyo…!

**BRIDGE MUSIC**

**SCENE 6: MARIA'S HOUSE**

**84.** ***SFX: KITCHEN NOISES. POTS AND PANS***

**85. CHEMU** ***(giggling)*** Sam, fanya upesi... sitaki mama ajue tunakunywa mchuzi wake.

**86. SAM** Ohhh, hii supu ni tamu…!

**87. CHEMU** Tule !

**88. SAM** Lakini hii supu ni baridi…Kwanini tusiipashe moto?

**89. CHEMU** Tukiipasha moto, Mama atasikia harufu chumbani mwake na atajua tunakunywa supu yake.*(giggles)*

**90. SAM** Lakini afadhali nini? ...heee... Mamako ajue tunakunywa supu yake au kuambukizwa ugonjwa wa kuhara?

**91. CHEMU** Hapo umesema kweli. Nimesahau kwamba chakula cha baridi pia kinaweza kutuambukiza ugonjwa wa kuhara. Chakula hiki kimekuwa hapa bila ya kufunikwa kwa muda sasa.!

**92. SAM** Lazima tukipashe moto.

**93. CHEMU** Mama atakasirika, na kisha unamfahamu vyema.

**94. SAM** Ungetaka kujua watu wanavyosikia wanapougua kuhara?

**95. CHEMU** La hasha…! Nataraji Mama hatosikia harufu hii ya supu yake.

**BRIDGE MUSIC**

**OUTRO:**

**96. NARRATOR** SAM NA CHEMU BADO WANAENDELEA KUZIPA MSUKUMO HARAKATI ZAO. KWA SASA WAMESHAJIFUNZA MBINU MUJARAB ZA KUEPUKA MAAMBUKIZI YA UGONJWA WA KUHARA NYUMBANI KWAO. PIA WAMEFAULU KUWASHAWISHI WAZAZI WAO KUHUSU UMUHIMU WA KUWASIKILIZA NA KUSHIRIKIANA NAO.

KWA UPANDE MWENGINE BADO WANA CHANGAMOTO SHULENI MWAO ZA KUJIKINGA NA MAAMBUKIZI NA NJIA ZA KUZUWIA KUSAMBAA UGONJWA WA KUHARA.

USIKOSE KUUNGANA NASI TENA KWA MAKALA YAJAYO YA NOA BONGO WAKATI SAM NA CHEMU WANAPOREJEA SHULENI NA KUANZA AWAMU TOFAUTI YA KIBARUA CHAO…..

UKIPENDA KUKISIKILIZA TENA KIPINDI HIKI NA VYENGINE VINGI VINAVYOTAYARISHWA NA DEUTSCHE WELLE AU AU KUTUMA MAONI, TEMBELEA MTANDAO WETU WWW.DW-WORLD.DE/LBE. HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.